PRE-MOCK PRE-MOCK PRE-MOCK PRE-MOCK PRE-MOCK PRE-MOCK PRE-MOCK PRE-MOCK PRE-MOCK PRE-MOCK PRE-MOCK PRE-MOCK

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA TAMISEMI

HALMASHAURI YA MJI KIBAHA

MTIHANI WA KABLA YA UTIMILIFU KIDATO CHA PILI

021 **KISWAHILI**

MUDA: MASAA 2:30 **MWAKA:2024**

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali 10.
2. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
3. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

KWA MATUMIZI YA MSAHIHISHAJI TU		
NAMBA	ALAMA	SAINI YA MSAHIHISHAJI
1		
2		
3		
4		
5		
6		
7		
8		
9		
10		
JUMLA		

SEHEMU A (ALAMA 15)

1. Chagua jibu sahihi katika vipengele (i)-(x), kisha andika herufi ya jibu hilo kwenye karatasi ya kujibia

   i. Amani alimwambia Joyce kuwa "ili uwe mahiri wa lugha ya mazungumzo huna budi kuwa mtumwa huru katika lugha husika" ukiwa kama mtaalamu wa lugha ya Kiswahili unahisi Amani anamaanisha nini kwa Joyce?
   A. Kutenga vifungu vya sentensi ambazo ni ndefu
   B. Joyce awe anazingatia mandhari, ujumbe, dhamira, mada
   C. Joyce awe anazingatia mada, lengo la mazungumzo, uhusihano baina ya wazungumzaji, muktadha
   D. Joyce awe anazingatia uhunzi, uhusiano, umri, lengo la mazungumzo

   ii. Uundaji wa maneno unatumia njia mbalimbali. Neno **Pundamilia** limeundwa kwa njia ipi kati ya hizi zifuatazo?
   A. Njia ya uradidi
   B. Njia ya uambatanishaji
   C. Njia ya mnyumbuliko
   D. Njia ya ukopaji

   iii. Kuna wakati watumiaji wa lugha hufanya makosa pasipo kukusudia. Sentensi isemayo "mwalimu mkuu aliwakilisha barua kwa Mkurugenzi wa Mji" sentensi hii inakosa gani la kisarufi?
   A. Kosa la kimuundo
   B. Kosa la kimsamiati
   C. Kosa la kimatamshi
   D. Kosa la kimaana

   iv. Mwalimu Mussa aliwapa wanafunzi wake kamusi za Kiswahili, kisha akawaambia wabainishe umuhimu wa kamusi katika Lugha. Jifanye wewe ni Miongoni mwa wanafunzi hao. Je ni umuhimu upi ambao hautaupata katika kamusi?
   A. Kujua matamshi ya neno
   B. Kujua kategoria ya neno
   C. Kujua aina ya sentensi
   D. Kujua maana ya neno

   v. "Napenda kujibu swali la nyongeza la muheshimiwa kama ifuatavyo", "Mimi kuku wali", "Zuia babu kula vichwa vitatu". Mtindo huu wa Lugha una faida gani kwa jamii?
   A. Kufanikisha mawasiliano
   B. Kutofautisha waandishi
   C. Kujipatia huduma
   D. Kupamba lugha

   vi. Atugonza amekwenda **Kagera**. Neno lilopigiwa mstari katika sentensi hii ni aina gani ya neno
   A. Kiwakilishi
   B. Nomino
   C. Kielezi
   D. Kihusishi

vii. Mama Nyanjiga alisema, **Flora ni msichana mzuri sana**. Wewe ni mwanafunzi wa kidato cha pili uliye mahiri wa lugha na unayejua alama za uandishi. Unafikiri alama gani ya uandishi ingefaa katika sentensi iliyokolezwa?

A. Ritifaa
B. Kiulizo
C. Alama za mtajo
D. Mabano

viii. Chakula kitaletwa kutoka kijijini. Sentesi hii ipo katika wakati gani?

A. Hali ya mazoza
B. Timilifu
C. Uliopita
D. Ujao

ix. Kinyogori ni mchina anayetaka kujua dhana ya ufahamu. Katika seti zifuatazo msaidie kinyogori kubaini fasili ya ufahamu iliyo sahihi

A. Kujua, kufikilia na kuelewa jambo na vitu
B. Kusoma, kusikiliza na kutafakari
C. Kujua, kuelewa na kuweza kufafanua jambo
D. Kuona, kusikiliza na kutafakari

x. Neno **shurutishwa** limeundwa na silabi ngapi?

A. Nne
B. Tano
C. Sita
D. Tatu

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.

2. Oanisha kifungu cha maneno toka orodha A na kifungu cha maneno toka orodha B ili kupata jibu sahihi

	ORODHA A	**ORODHA B**
i.	Huonesha mpangilio wa maneno kialfabeti jinsi yanavyoandikwa, yanavyotamkwa na maana zake	A. Tanzu za lugha
ii.	Lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi	B. Rejesta
iii.	Maneno yasiyo sanifu yanayozungumzwa na kikundi kidogo cha watu	C. Simo
iv.	Taaluma inayoshughulikia maumbo au mjengo wa maneno katika tungo	D. Sarufi maumbo
v.	Ni mtindo wa lugha unaozungumzwa kulingana na muktadha na kusudi maalum.	E. Misemo
		F. Nomino
		G. Mofimu
		H. Kamusi
		I. Sarufi maana

ORODHA A	i.	ii.	iii.	iv.	v.
ORODHA B					

SEHEMU B (ALAMA 70)

Jibu maswali yote kwenye sehemu hii.

3. Kuna mambo ya msingi au muhimu yanayopaswa kuzingatia wakati wa kutoa fasili au maana ya lugha. Ukiwa kama nguli wa Kiswahili eleza mambo matano ya msingi yanayopatikana kwenye maana ya lugha

   i. ……
   ……
   ……

   ii. ……
   ……
   ……

   iii. ……
   ……
   ……..

   iv. ……
   ……
   ……

   v. ……
   ……
   ……

4. (a) Toa mfano mmoja kwa kila kielezi cha namna kifuatacho

   i. Kielezi cha namna kiingizi
   ……

   ii. Kielezi cha namna kikariri
   ……..

   (b) Bainisha hisia zilizomo katika vihisishi vifuatavyo

   i. Loo jamani!
   ……..

   ii. Aha wapi!
   ……..

   iii. Umeona ee!!
   ……

(c) Badili vitenzi vifuatavyo viwe katika kauli ya kutendeka

i. Fika ……..…..……

ii. Zoa ……..……..……

iii. Komboa ……..……

iv. Omba ……

v. Zuia ……..……..

5. (a) Ashura alienda kununua kamusi, alipoifungua kamusi hiyo alitahamaki kukuta picha na michoro mingi katika kamusi, hivyo aliomba abadilishiwe apewe kamusi isiyo na picha na michoro kwani hakuna faida ya picha na michoro katika kamusi. Wewe kama mwanafunzi wa kidato cha pili taja faida tano za michoro na picha katika kamusi.

i. ……

ii. ……

iii. ……..

iv. ……..……

v. ……..…….

(b) Kwakutumia mifano, Eleza maana ya maneno yafuatayo

i. Irabu

……

……

……

ii. Rejesta

……

……

……

iii. Takriri

……

……

……

iv. Methali

……

……

……

v. Lugha

……

……

……

6. (a) Eleza dhima za kiambishi "NI" kilichopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo.

i. Foibe <u>ni</u> mchoyo

……

ii. Ninakwenda nyumba<u>ni</u>

……

iii. Wame<u>ni</u>choma
……..

iv. <u>Ni</u>naimba wimbo mzuri
……..

v. Ana<u>ni</u>omba mara kwa mara
……..

(b) Taja kwa mifano miundo mitano ya silabi

i……

……

ii……..

……

iii……

……

iv……

……

v……

……

7. (a) Mwandishi yeyote yule lazima azitambue sifa pambanuzi za fasihi simulizi. Bainisha sifa tano (5) za fasihi simulizi.

i. ……..……
……..

ii. ……
……

iii. ……..……
……..

iv. ……..……
……..

v. ……
……

(b) Mbali na fasihi, taja aina nyingine tano (5) za Sanaa.

i……

ii……...

iii……..

iv……..

v……
…

8. (a) Kwakutoa mifano thabiti, fafanua vyanzo vitano vya Misimu.
   i. ……
   ……
   ii. ……
   ……
   iii. ……..……
   ……..
   iv. ……
   ……..
   v. ……
   ……..

   (b) Misimu ina umuhimu wake katika jamii, kwa kutoa mifano taja faida tano za misimu.
   i. ……
   ……
   ii. ……
   ……
   iii. ……
   ……
   iv. ……
   ……
   v. ……
   ……
9. (a) Ukiwa mwanafasihi mzuri, toa maana ya nahau zifuatazo kwa kuandika maana mbele ya nahau husika.
   i. Ana mkono mrefu.
   Maana yake ni……
   ii. Amevaa miwani
   Maana yake ni……
   iii. Ana mkono wa birika
   Maana yake ni……
   iv. Pata jiko
   Maana yake ni……
   v. Zunguka mbuyu
   Maana yake ni…….

   (b) Kamilisha methali zifuatazo

i. Kuishi kwingi……………………………………………………………………………………..

ii. Chanda chema………………………………………………………………………………

iii.Asiyekubali kushindwa………………………………………………………………………….

iv.Jambo usilolijua……………………………………………………………………………….

v.Mwenda tezi na omo……………………………………………………………………………..

SEHEMU C (ALAMA 15)

10. Baba yako anafanya kazi ya mwalimu Mkuu wa shule ya sekondari Azimio S.L.P 10 Mwanza, mwandikie barua ukiomba pesa ya matumizi binafsi uwapo shuleni. Jina lako liwe Amani Simba.

……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……
……………………………………………………………………………………………………
……
……
……
……
…………………………………………………………………
……
……
……
……
……
……
……………………………………………………………………………………………………
……
……
……
……

.....
.....
.....
.....